



(Imesajiliwa nchini Tanzania chini ya Sheria ya Kampuni ya Tanzania namba 212 ya mwaka 2002 kama kampuni yenye dhima ya ukomo, cheti cha usajili namba 103309)

TAARIFA KWA UMMA

ITRUST EAC LARGE CAP ETF: UREKEBISHAJI UPYA WA MALI KWA AJILI YA ROBO YA KWANZA (Q1) 2026

iTrust Finance Limited inapenda kutoa taarifa kwa umma kwamba, kwa mujibu wa Kifungu cha 17.7 cha Mkataba wa Uendeshaji wa Mfuko wa iTrust EAC Large Cap Exchange Traded Fund, Mfuko umefanya urekebishaji (rebalancing) wa robo ya kwanza (Q1) ya mwaka 2026 kwa kuzingatia mfumo uliopitishwa wa uwekezaji na mgawanyo wa rasilimali. Urekebishaji huo unahusisha marekebisho ya uzito wa dhamana zilizochaguliwa ndani ya mfuko pamoja na kuingizwa kwa dhamana mpya inayostahiki, kwa lengo la kudumisha ulinganifu na mamlaka ya Mfuko na kuhakikisha kuendelea kwa uzingataji wa Mkataba wa Uendeshaji na mahitaji ya kisheria na kanuni za udhibiti zinazotumika..

MUHTASARI WA UREKEBISHAJI WA MFUKO

Urekebishaji huu unajumuisha kuingizwa kwa Stanbic Holdings Plc Kenya (SBIC) kwa uzito wa 3.50%; hisa iliyoorodheshwa katika Soko la Hisa la Nairobi (NSE), pamoja na marekebisho ya uzito wa baadhi ya dhamana zilizopo katika Kenya, Tanzania na Uganda, kwa lengo la kuboresha ukwasi wa mfuko, urahisi wa uwekezaji, na kuimarisha mseto wa uwekezaji. Mabadiliko kwa muhtasari yameainishwa katika jedwali hapa chini:

HISA	UZITO UNAOLENGWA SASA	UZITO MPYA UNAOLENGWA	% MABADILIKO
Stanbic Bank Kenya	-	3.50%	+3.50%
Tanzania Portland Cement	5.49%	3.99%	-1.50%
Vodacom Tanzania	5.85%	3.85%	-2.00%
Kenya Commercial Bank	11.14%	12.14%	+1.00%
Stanbic Bank Uganda	3.36%	2.36%	-1.00%



UFAFANUZI

Wawekezaji wanaohitaji ufafanuzi zaidi wanashauriwa kuwasiliana na washauri wao wa uwekezaji au iTrust Finance Limited kupitia barua pepe: info@itrust.co.tz, au simu +255 659 071 777, kwa ajili ya maelezo zaidi.

SHUKRANI

Uongozi wa iTrust Finance Limited unapenda kuwashukuru taasisi zote zilizowezesha utekelezaji wa urekebishaji huu wa mfuko. Taasisi hizo ni pamoja na Bodi na uongozi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); Mwangalizi NBC Bank PLC pamoja na Mshauri wa Kisheria Vertex Law Chambers.

Imetolewa na:

**Afisa Mtendaji Mkuu, iTrust Finance Limited,
S. L. P. 22636, 429 Mahando Street, Masaki, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 659 071 777, Barua pepe: info@itrust.co.tz, Tovuti: www.itrust.co.tz
Tarehe: 27 Aprili 2026**

Tangazo hili limetolewa kwa idhini ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa mujibu wa kanuni za Masoko ya Mitaji za Matangazo, G.N. Namba. 15 ya mwaka 1997.